MAMLAKAYA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA (TFRA)

MAELEZO KUHUSU MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA (BPS - FERTILIZER BULK PROCUREMENT SYSTEM)

2017

1. UTANGULIZI

Tanzania ni nchi mojawapo barani Afrika kusini mwa jangwa la Sahara yenye matumizi ya chini sana ya mbolea katika ngazi ya wakulima wadogo. Azimio la Maputo *(The Maputo declaration, 2003)* liliazimia masuala mbalimbali katika kilimo, pamoja na mambo mengine; kuongeza matumizi ya mbolea katika eneo la ukanda wa SADC kufikia angalau kilo 50 za virutubisho kwa hekta (kwa sasa Tanzania imefikia kiwango cha kilo 19 za virutubisho kwa hekta ambayo ni sawa na asilimia 38 ya lengo).

Aidha matumizi haya yamekuwa changamoto kubwa kwa tasnia ya mbolea na serikali. Kwa miaka hamsini iliyopita Wzara ya Kilimo imekuwa ikiweka mikakati na mifumo mbalimbali yenye lengo la kuongeza matumizi na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji wenye tija.

Ikiwa ni Mkakati mmojawapo wa kupunguza bei ili kuhamasisha matumizi ya mbolea nchini, Serikali kwa kushirikiana na wadau wake iliandaa Kanuni za kusimamia ununuzi wa mbolea kwa pamoja *(Fertilizer (Bulk procurement) Regulations)* ambazo zilitangazwa katika gazeti la Serikali Namba 49 mnamo Februari 17, 2017. Kanuni hizi ziliundwa chini ya Kifungu cha 51 cha Sheria ya mbolea namba 9 ya mwaka 2009. Lengo la kanuni hii ni kusimamia na kuratibu mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja *(BPS - Bulk Procurement System)* chini ya Wizara ya Kilimo kupitia taasisi yake iitwayo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania *(TFRA - Tanzania Fertilizer Regulatory Authority).*

Kanuni hizi zinapatikana katika tovuti ya Wizara na unaweza kuzipata kwa kutembelea http://www.kilimo.go.tz/index.php/en/resources/category/regulations.

2. CHANZO CHA MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA NCHINI

Katika miaka ya 2000 na mwanzoni wa mwaka wa 2010, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia *(World Bank)* na wadau wengine wa maendeleo *(Development partners*), ilianzisha na kutekeleza mpango wa vocha za pembejeo za kilimo kwa mkulima hususan mbolea. Katika kipindi hicho mpango huo ulisaidia kuhamasisha na kutia chachu ya matumizi ya mbolea hapa nchini. Mbolea iliweza kupatikana kwa wakulima wanufaika kwa bei nafuu kufuatia punguzo la bei lililotolewa na Serikali kupitia ruzuku.

Katika zao la korosho, mfumo huu umewahi kutumika katika kuagiza mbolea na viuatilifu (Sulphur). Mfumo huu wa BPS ulikuwa na mafanikio makubwa kwani bei ya pembejeo ilishuka na hivyo kuwawezesha wakulima kutumia pembejeo zaidi.

Kwa upande mwingine, kwa dhamira njema ya serikali ya kuongeza matumizi ya mbolea kwa kwa kupunguza bei, Wizara iliendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika tasnia ya mbolea. Kwa mantiki hiyo mwaka 2006 serikali iliweka makubaliano na kampuni mojawapo kuagiza mbolea kwa pamoja *(bulk importation)* na iliwezeshwa na serikali kutumia miundombinu msingi *(basic infrastructure for investment)* katika eneo lililo karibu na Bandari (hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka wa fedha 2012/2013; kifungu cha 56, ukurasa wa 33-34). Miundombinu hiyo ni pamoja na maghala ya kutunzia mbolea na reli ya kusafirishia mizigo kutoka bandarini.

Uwekezaji wao ulikusudiwa kuongeza matumizi ya mbolea kwa wakulima na kuhamasisha ukuaji wa tasnia ya mbolea ili wakulima waweze kuipata kwa bei nafuu. Aidha, ilitarajiwa kwamba makampuni mengine yanayojishughulisha na mbolea hapa nchini kutumia fursa

hiyo kwa kushirikiana kwa karibu na kampuni iliyokubaliana na Serikali kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi.

3. SABABU ZA KUWEPO KWA MFUMO WA UNUNUZI YA MBOLEA KWA PAMOJA

Soko la mbolea ni la kimataifa kwa maana ya kwamba zaidi ya asilimia 90 ya mbolea yote inayotumika hapa nchini huagizwa kutoka nchi za nje. Kabla ya kuanza kwa mfumo wa BPS, kila mfanyabiashara aliyetaka kuingia katika soko hili alitakiwa kwanza kupata ufahamu wa soko la dunia la mbolea ikiwa ni pamoja na kujua viwanda vya mbolea, kujua bei za mbolea, kujua ubora wa mbolea zinazofaa katika ardhi za Tanzania.

Kwa hakika ni gharama kubwa sana kuliko kulifahamu soko kwa bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini kama Sukari. Kutokana na ukweli huo wa msingi, bado Tanzania ina ushindani mdogo sana katika soko la mbolea ambao unafanya bei zake kuwa juu. Kwa kipindi cha miaka 15 hivi iliyopita, sekta binafsi imeshiriki katika mnyororo wa thamani wa mbolea *(fertilizer value chain)* hapa nchini, hivyo kuongeza upatikanaji na ushindani kwa kiasi fulani katika biashara ya mbolea.

Pamoja na ushiriki wa makampuni kadhaa, bado ushindani uko chini na hivyo kufanya bei ya mbolea kwa soko la ndani ni mdogo na hivyo bei ya mbolea imeendelea kuwa kuwa juu. Aidha, mengi ya makampuni haya huagiza mbolea kwa kiwango kidogo na hivyo kufanya gharama za uagizaji *(importation overhead cost)* kuwa kubwa.

Kutokana na hali hii, Serikali ilifikia maamuzi ya kumtumia mwingizaji mmoja anayelifahamu vizuri soko la dunia la mbolea.

4. HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KUPUNGUZA BEI YA MBOLEA HAPA NCHINI

Baada ya serikali kuondoa mfumo wa ruzuku kwa njia ya vocha *(National Agricultural Input Voucher Scheme),* Serikali imechukuwa hatua mbalimbali zilizo endelevu ili kuongeza matumizi ya mbolea na kupunguza bei kwa mkulima

4.1. Kufanya mapitio ya Kanuni ya mbolea ya mwaka 2011

Fertilizer (Amendments) Regulations, GN no 50/2017)

Ili kufikia lengo la kusimamia bei ya mbolea serikali kwa kushirikiana na wadau wake ilirekebisha Kanuni hizo ili kuruhusu wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea kuweka **bei elekezi** katika mbolea zinazouzwa kwa wakulima.

4.2. Kupunguza gharama za usafirishaji wa mbolea kutoka Bandarini hadi kwa mkulima

Usafirishaji wa mbolea kutoka Bandari ya Dar es salaam kwenda mikoani kwa mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (BPS) unamtaka msambazaji wa mbolea atumie njia ya reli pekee hususani katika maeneo ambayo usafiri wa reli unapatikana. Mikoa yote yenye mtandao wa reli ama TAZARA au Reli ya kati (TRL) ambako kuna matumizi makubwa zaidi ya mbolea; mfano Nyanda za juu kusini hutumia asilimia 62 ya mbolea zote zinazotumika hapa nchini. Njia ya barabara itatumika tu mahali ambapo hakuna reli; wilayani na vijijini. Kwa kutumia njia ya reli gharama ya usafirishaji itapungua kwa asilimia 60 ikilinganishwa na njia ya barabara. Aidha, ikumbukwe kwamba treni ina uwezo wa kubeba mzigo mkubwa zaidi wa mbolea na kwa wakati mfupi ilinganishwa na njia ya barabara. Kwa kuzingatia kuwa

usafirishaji unachukua sehemu kubwa katika mjengeko wa gharama za mbolea, ni vyema tukaona umuhimu wa kutumia njia ya reli ili kupunguza gharama ya mbolea kwa mkulima.

4.3. Kuanzisha mfumo wa ununuzi ya mbolea kwa pamoja *(Fertilizer (Bulk Procurement) Regulations, 2017 (GN No.49/2017)*

Moja ya mifumo iliyopendekezwa na serikali kwa kuzingatia uzoevu na uchambuzi wa taarifa mbalimbali za awali *(previous fertilizer delivery system study reports)* imeamua kutumia mfumo wa manunuzi ya mbolea kwa pamoja ambao utasaidia kupunguza gharama za uaendeshaji *(overhead costs)* katika ununuzi na usafirishaji wa mbolea.

5. JINSI MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA UNAVYOFANYA KAZI

Kanuni za Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja *(The Fertilizer (Bulk Procurement) Regulations, 2017)* zinaelekeza kwamba uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi lazima ufanyike kupitia utaratibu ulioainishwa ambao ni kwa kutangaza zabuni kwa ushindani *(competitive bidding)* na kwamba mfumo uko wazi kwa kila mtu kushiriki na zabuni hiyo inafanyika kwa uwazi kwa kuzingatia taratibu zilizoainishwa katika Kanuni hizo na mwongozo wa usimamizi wa utekelezaji wa mfumo huo.

Aidha, kwa msimu 2017/2018 mfumo huu utaanza kwa kuagiza aina mbili tu za mbolea ambazo ni; mbolea ya kupandia *(DAP)* na mbolea ya kukuzia *(UREA)* na mbolea zingine zitafuata baadaye kadri itakavyoonekana mfumo huu umeleta manufaa kwa mlaji. Kwa mantiki hii mbolea zingine zote (NPK, CAN, SA, MOP, TSP, blends mbalimbali, Biofertilizers na zile za maji "foliar") zitaendelea kuletwa kwa utaratibu wa zamani.

Bei za mbolea zitatangazwa na Serikali kupitia Wizara katika vyombo vya habari kama vile magazeti, redio na Luninga.

6. FAIDA ZA MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA

i. Mfumo huu utasaidia kuimarisha utaratibu wa usambazaji wa mbolea ambapo wadau wote watapata uhakika wa upatikanaji wa mbolea kwa bei ya ushindani katika soko kwa kununua mbolea kutoka kwa mwagizaji aliyepatikana kwa ushindani kupitia zabuni ya ununuzi wa mbolea kwa pamoja.

ii. Kuwezesha wafanyabaishara wadogo wa mbolea kukua na kushiriki katika biashara ya mbolea na hivyo kuimarisha mtandao wa usambazaji hadi ngazi ya mkulima, kuongeza upatikanaji na kupunguza bei ya mbolea.

iii. Kudhibiti bei ya mbolea iwapo kutajitokeza ongezeka lisilikokuwa na sababu "soko holela". Bei itatangazwa kwa kuzingatia bei halisi ya mbolea, gharama halisi za uasafrishaji wa mbolea, tozo mbalimbali na kiwango stahiki cha faida ya mfanya biashara.

7. MAJUKUMU YA HALMASHAURI

Suala la BPS linahitaji ushirikiano wa hali ya juu kati ya Mamlaka ya mbolea na halmashauri kwani shughuli zote za Kilimo ziko chini yake. Ili kuwezesha hili, halmashauri ina wajibu ufuatao: -

i. Kuhamashisha wakulima kutumia mbolea kwa kiasi na viwango vya ubora vinavyopendekezwa na wataalam wa kilimo

ii. Kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha kwamba mbolea inayotumiwa na wakulima inakidhi viwango vya ubora.

iii. Kukusanya takwimu kuhusu aina, kiasi kilichotumika na kilichobaki ghalani.

iv. Kukusanya takwimu za bei ya mbolea kwa wakala na wakulima.

v. Kutoa taarifa kwa TFRA kuhusu suala lolote linalohusu tatizo la mbolea iliyo chini ya viwango inayoweza kuathiri tija na uzalishaji wa mazao.

8. HITIMISHO

Muundo wa kisheri wa kusimamia ununuzi wa mbolea kwa pamoja umekamilika na nyaraka hizo zitatumika kusimamia utekelezaji wa mfumo huu katika msimu wa kilimo wa 2017/2018 kwa kuanza na mbolea ya kupandia (DAP) na mbolea ya kukuzia (UREA). Kupitia mfumo huu inatarajiwa matokeo chanya katika kupunguza bei ya mbolea kwa mkulima mdogo na hivyo kuwezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini. Kwa kuzingatia hayo Serikali inawaomba wadau wote kushiriki kikamilifu kuunga mkono juhudi za serikali za kushusha bei ya mbolea na kuongeza matumizi yake hapa nchini ili kutimiza azma ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga nchi ya uchumi wa viwanda ambapo sekta ya kilimo itatoa mchango mkubwa kwa manufaa ya taifa zima.